**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUSHIKILIWA KWA WAKILI MENRAD D'SOUZA**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umesikitishwa na taarifa za kushikiliwa kwa Wakili Menrad D'Souza pamoja na wateja wake huko Babati mkoani Manyara. Wakili D'Souza alifungiwa katika chumba kwenye ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Manyara juzi tarehe 30/07/2018 kwa kile kinachodaiwa ni kumshinikiza wakili na wateja wake waweze kuwasiliana na wakurugenzi wa wateja hao ili wakubali kuongeza kiasi cha fidia kwa wakulima katika mgogoro wa mbegu kati ya wakulima na wateja wa Wakili D'Souza. Baada ya kufungiwa kwa muda taarifa zilisambaa katika mitandao ya kijamii na baadae wakili pamoja na wateja wake walishikiliwa na polisi kwa tuhuma za uchochezi.

Baada ya taarifa za kushikiliwa kwa wakili huyo kusambaa, mawakili wakiongozwa na Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) walifanya juhudi mbalimbali za kusaidia kuachiwa huru kwa wakili huyo na baadae walilifikisha jambo hilo mahakamani kuomba mahakama iamuru wakili huyo afikishwe mahakamani na kusikilizwa (Habeas Corpus) au kuachiwa kwa dhamana ya polisi. Kufikia jana jioni tarehe 31 Julai 2018 wakili huyo aliachiwa huru.

THRDC kama mwavuli wa watetezi wa haki za binadamu Tanzania inatambua kuwa mawakili ni watetezi wa haki za binadamu na wanafanya kazi zao za utetezi kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na nchi. Msingi wa kazi za mawakili unatoka katika Katiba ya jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Mawakili (Cap 341), Mikataba ya Kimataifa na pia mikataba ya kikanda iliyosainiwa na serikali ya Tanzania. Kwa mujibu wa kifungu cha 66 cha sheria ya Mawakili, Wakili ni Ofisa wa Mahakama. Hivyo mawakili wanastahili kupewa ulinzi na uhuru wa kufanya kazi zao pasipo kuingiliwa na mamlaka za serikali ili waweze kusaidia kutoa haki.

Itakumbukwa kuwa huko nyuma Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania umewahi kukemea vitendo mbalimbali vya uvunjifu wa haki za binadamu kwa mawakili na watetezi wengine wa haki za binadamu. Mnamo tarehe 12 Septemba 2017 Mtandao ulitoa tamko kulaani vikali kuvamiwa kwa

ofisi za Mawakili za Prime Attorneys jijini Dar es Salaam pamoja na tukio lingine la kulipuliwa kwa ofisi za mawakili za IMMMA Advocates lililotokea Agosti 26, 2017.

Katika miaka ya hivi karibuni matukio haya ya uvunjifu wa haki za mawakili yamekua yakiongezeka kwa kiasi kikubwa. Mawakili wamekua wakiingiliwa katika kazi zao, kukamatwa na mara kadhaa maofisa wa serikali wamekua wakitoa matamko yanayosababisha kuminywa kwa uhuru wa mawakili. Mfano, Mnamo tarehe 22 Julai 2016 wakili wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Shilinde Ngalula alikamatwa na Polisi akiwa katika kutekeleza majukumu yake ya kiwakili huko Loliondo. Kukamatwa kwake kulifuatia tuhuma za uchochezi zilizotolewa dhidi yake na kuunganishwa kwenye kesi ya wateja wake waliokuwa wakituhimiwa kuwa ni majasusi na wachochezi. Matukio ya uvunjifu wa haki za mawakili yamekua yakitokea pia Zanzibar ambapo watu wasiojulikana walivamia offisi za mawakili na kupotea kusikojulikana. Pia Polisi Visiwani Zanzibar walinukuliwa mwaka 2016 wakiwatishia mawakili hasa wanaotetea wananchi visiwani Unguja na Pemba kuwa wataunganishwa na kesi hizo za wananchi kama wahalifu endapo watawatetea.

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu unaona kwamba madhara ya vitendo hivi yatakuwa ni makubwa na wananchi watashindwa kupata haki yao ya kupata huduma na msaada wa kisheria kutoka kwa mawakili iwapo vitendo hivi vitaendelea.

**Wito wetu**

Ikumbukwe kwamba tabia hii ya kuwashikilia watuhumiwa kwa muda mrefu na baadae kuwaachia huru baada ya watuhumiwa kupeleka maombi mahakamani ya kutaka kuachiliwa na/ama kupewa dhamana ya polisi,imekuwa ikijirudia mara kwa mara. Kutokana na kitendo hicho cha Mkuu wa mkoa na Polisi mkoani Manyara, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania unapenda kutoa mapendekezo yafuatayo.

- Tunaomba wakuu wa mikoa na wilaya nchini kuacha kutumia madaraka yao chini ya Kifungu cha 15 na 17 cha Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1996 kwa kutoa amri za kuwakamata watu na kuwaweka vizuizini bila sababu za msingi na za kisheria.
- Tunalishauri Jeshi la polisi kuacha utaratibu wa kuwashikilia watuhumiwa kwa muda mrefu bila kuwafikisha mahakamani na baadae kuwaachia huru au kuwapa dhamana baada ya watuhumiwa au

mawakili wa watuhumiwa kufungua kesi mahakamani ya kuiomba Mahakama itoe amri ya kuletwa kwa mtuhumiwa ili aweze kusikilizwa (Habeas Corpus). Tunawakumbusha Jeshi la Polisi kuwa wanapaswa kukaa na watuhumiwa katika mahabusu kwa muda usiozidi masaa 48 kwa kua wao hawana vifaa, majengo wala vyakula vya kuwalisha watuhumiwa endapo watakaa kwa muda mrefu. Mtakumbuka kilichompata Mtetezi wa Haki za Binadamu Abdul Nondo aliyeshikiliwa na Polisi kwa muda wa siku 19 bila kufikishwa mahakamani au kupewa dhamana. Tabia hii inapaswa kukemewa na wapenda haki wote.

- Maafisa wa serikali na jamii kwa ujumla itambue na kuheshimu kazi za mawakili nchini kwani wanafanya kazi zao za utetezi wa haki za binadamu kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi. Tunashauri kwamba ikitokea kuna wakili kiongozi anadhani amekiuka maadali ya kazi yake basi atoe taarifa kwa chama cha mawakili au Mahakama.
- Tunawasihi mawakili wote na pia kupitia vyama vyao wasimame kwa umoja na kulinda uhuru wa kazi ya mawakili na utawala wa sheria hapa nchini

- Tunawashauri viongozi wetu wa sasa kuzingatia sana utawala wa sheria, misingi ya haki za binadamu, uhuru wa makundi ya watetezi na mgawanyo wa madaraka wanapokuwau wanatekeleza majukumu yao.

**Imetolewa leo tarehe 01 August 2018**

**Na**



**Onesmo Olengurumwa**

**Mratibu; Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**